# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.
## OFISI YA RAIS –TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
## HALMASHAURI YA MJI - TARIME
## SHULE YA SEKONDARI KENYAMANYORI

S.L.P 224,
**TARIME.**

15/12/2020

**KUMB.NA.KSS/JOIN/2021**.

**SIMU**: *0767115223/0787115221 (MKUU WA SHULE)*
*0756 860 925/0626991022 (MAKAMU)*
**Baruapepe:** sekenyamanyoriss@gmail.com

Jina la Mwanafunzi.........................................................
S.L.P ............

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KENYAMANYORI KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021.**

### 1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukutaarifu kuwa, umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii kwa mwaka 2021. **Hongera sana** kwa kupata bahati hii kubwa, ambayo vijana wengi kwa sasa wanaihitaji sana! Uongozi wa shule unakutakia maandalizi mema ya kuja kujiunga na shule hii, karibu sana. Shule ya sekondari Kenyamanyori ipo umbali wa **Km 11** mashariki mwa mji Mkuu wa Halmshauri ya Mji wa Tarime, katika **Kata ya Kenyamanyori** mtaa wa **Makao.** Usafiri wa kufika shuleni ukitokea mjini ni mwingi sana,upo usafiri wa pikipiki kwa nauli ya 2000/= na magari binafsi. Muhula wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti itakuwa tarehe 25/01/2021 ndani ya wiki mbili. Zingatia muda huu ili usije poteza nafasi adimu na muhimu katika maisha yako.

### 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

#### 2.1. Sare ya Shule:

#### 2.1.1 Wavulana.

- Shati mbili nyeupe za mikono mifupi zenye kuachia mwili na mfuko mmoja kushoto ziwe jozi mbili.
- Suruali rangi ya ugoro, mashono ya kawaida iwe na marinda mawili kila upande, isiwe modo iwekewe pindo(turn up) chini na iwe na mifuko mitatu tu ziwe jozi (pair) mbili. **Akishona tofauti atarudishwa nyumbani ili airekebishe**.
- Viatu vya ngozi vyeusi vyenye visigino vifupi.
- Soksi nyeusi jozi mbili
- Sweta rangi ya bendara ya Taifa lenye nembo ya shule yanapatikana mjini kwa wingi sana.
- Nembo ya shule
- Tai ndefu rangi ya ugoro.

#### 2.1.2. Wasichana:

- Sketi rangi ya ugoro kitambaa cha suti Namba 1, yenye marinda mapana ndefu inayokaribia usawa wa vifundo vya miguu. **Akishona vinginevyo atarudishwa nyumbani akairekebishe,** ziwe jozi mbili.
- Shati mbili nyeupe za mikono mifupi.
- Viatu vya ngozi nyeusi visigino vifupi
- Soksi nyeupe ndefu
- Sweta rangi ya Taifa
- Kwa waislam hijab inayo fanana na sare za shule
- Nembo ya shule
- Tai ndefu inayofanana na rangi ya sketi

**2.1.3 Sare za michezo**

- Viatu aina ya raba rangi nyeupe
- T-shirt rangi ya bluu isiyo na kola.
- Track suit rangi ya light blue

2.1.4 Daftari aina ya counter book (10), Kalamu na mathematical set(mkebe wa Hesabu)

2.1.5 Chakula cha wanafunzi wa kutwa kitapangiwa utaratibu siku ya kufungua, kutakuwa na kikao chao wazazi siku moja baada ya kufungua tarehe 12/01/2021 pamoja na matibabu ya mtoto yatagharamiwa na mzazi.

2.1.6 Kamusi ya kiingereza/Kiswahili (English- Swahili Dictionary).

2.0 Mahitaji mengine ya kibinadamu yatagharimiwa na mzazi/mlezi

**3.0 VIFAA VYA USAFI**

Mwanafunzi anatakiwa kuja na Mfagio mgumu (chelewa) kwa ajili ya usafi nje ya madarasa,.

**4.0 Sheria na kanuni muhimu za shule.**

6.3.1 Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
c. Kushiriki kikamilifu katika shughuli za kitaaluma darasani na nje ya darasa.
d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
g. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
i. Kukaa kwa utulivu unapokuwa darasani.

**5.0 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ukafukuzwa shule:**

a. Wizi.
b. Uasherati na ushoga.
c. Ubakaji
d. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k.
e. Kupigana au kupiga.
f. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g. Kudharau Bendera ya Taifa h. Kuoa au Kuolewa
i. Kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule.
j. kulala nje ya shule bila taarifa
k. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l. Kutukana watu kwa makusudi.
m. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi au vitu vinavyohusiana na simu.
n. Kukosa shule kwa siku 90 mfululizo bila taarifa rasmi.
o. Kuchelewa kufika shuleni kutoka likizo au unaporuhusiwa kutoka nje ya shule.
p. Utoro
q. Kuongoza au kuchochea mgomo
r .Kugomea maelekezo halali ya shule mfano kazi,chakula,masomo n.k

**6.0** **Ni marufuku** mwanafunzi kumiliki simu na vifaa vingine vya anasa, kufuga kucha/nywele na kusuka au kuweka nywele dawa.

**7.0 MAMBO MENGINE MUHIMU.**

Medical examination form ijazwe na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali, fomu za kukubali kujiunga na shule na kuendelea na masomo hadi kumaliza ya mzazi pamoja na mwanafunzi zimeambatishwa, fomu hizi zote zijazwe kikamilifu na kurudishwa shuleni siku ya kuripoti zikiwa ndani ya jarada la plastiki **(File).**

NB: **Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni akiwa na nakala ya cheti cha kuzaliwa.**

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.

……………………….

**ZEPHANIA NGALLA JOLIJO**
**MKUU WA SHULE.**

HEADMASTER
KENYAMANYORI SEC. SCHOOL
P.O. Box 224 TARIME.

***OR – TAMISEMI***

***HALMASHAURI YA MJI TARIME***

**SHULE YA SEKONDARI KENYAMANYORI**

**FOMU YA KUKUBALI SHULE**

## A. SEHEMU YA MWANAFUNZI

1. Mimi (Majina kamili) ………………………………………………………………..
   Nimekubali kuingia kidato cha …………………katika Shule ya Sekondari Kenyamanyori

   kuanzia tarehe ……………………………hadi nitakapomaliza kidato cha ………………….

2. Naahidi kwamba nitatii sheria za Shule na kushiriki katika shughuli zote za shule kikamilifu kulingana na ratiba.

3. Tarehe ya kuzaliwa……………………….Kijiji…………………………………..
   Tarafa…………………………………….. Wilaya ………………………………..
   Shule unakotoka ……………………………………….Namba yako ya mtihani shule ya msingi…………………………………….

4. Nikimaliza kusoma shule ningependa kufanya kazi ifuatayo ………………………
5. Ninawazazi wote/mzazi mmoja /Sina wazazi wote (yupo Baba/Mama) kata isiyostahili

   Sahihi ya mwanafunzi ……………………. Tarehe ………………………………...

## B. SEHEMU YA MZAZI AU MLEZI

1. Mimi (majina kamili) ……………………………………………………… simu……………………
   ninakubali mtoto wangu asome katika Shule ya Sekondari Kenyamanyori kuanzia kidato cha ……………………hadi atakapomaliza kidato cha ……………

2. Jina kamili la Mama ……………………………………………simu………………………………..
   Kazi ya Baba ………………………………………..

3. Kazi ya Mama ………………………………………
4. Anwani ya Mzazi/Mlezi ………………………………
   …………………………………………………………

   ……………………………………………………………

5. Wafuatao ni Ndugu zake ninaowatambua wanaweza kumsaidia wakati wa dharura

| Jina kamili | Mahusiano | Anakoishi | Simu yake |
|---|---|---|---|
| (i)…………………… | …………….. …… | ……………………. | …………… |
| (ii)…………………… | …………..………. | ……………………. | …………… |
| (iii)……………………. | ……………………. | ………………….. | …………… |

6. Madhehebu ya Dini ya Mtoto ni Lutheran/Katoliki/Anglican/PAG/TAG/ Moravian /SDA/Mwislam
7. Ripoti zote za maendeleo ya mwanafunzi ziwe zinatumwa kwa
   ………………………………………………………..

   ………………………………………………………..

   ………………………………………………………..

   Sahihi ya Mzazi/Mlezi

   Tarehe ……………………………………………..

## *KENYAMANYORI SECONDARY SCHOOL*

## *FORM FOR STUDENTS MEDICAL EXAMINATION*

To be completed by a Medical Officer

…………………………………………(Insert name of **the** Government Medical Institution)

Name of Student ………………………………………………. Form ………………… Year……….

Age ……………………………………………………………. Sex………………………………..

Blood count …………………………………………………………………………………….

Stool ………………………………………………………………………………………

Urine ……………………………………………………………………………………

T. B. Test ………………………………………………………………………………….

Eyes ……………………………………………………………………………………..

Ears ……………………………………………………………………………………

Chest ……………………………………………………………………………………..

Spleen …………………………………………………………………………………

Abdomen ……………………………………………………………………………

Teeth ……………………………………………………………………………………..

Additional information:- (***e.g. pregnancy, physical defects, infections, psychological disorder, chronic or family diseases*).**

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

**I certify that above pupil is fit to continue with studies in Secondary School for four years.**

Name of Medical Officer ……………………………………………Signature ……………………

Designation ……………………………………………

Station & Official Stamp………………………………….. Date ……………………….

***Sharti mtoto apimwe kikamilifu kabla ya daktari kujaza fomu hii. Ikigundulika kuwa daktari alijaza fomu hii bila vipimo kufanyika, wahusika watachukuliwa hatu za kisheria na za ukiukaji wa haki za binadamu.***